



KURUDI NYUMBANI 2019

Maelezo (information) kwa wakimbizi na wageni
kuhusu kurudi nyumbani kwa utashi wao

KAMA UNA NIA YA KURUDI NYUMBANI

Shirika ya Danemark ya msaada kwa wakimbizi inapanaka shauri kwa wakimbizi na wageni wenyi kupenda kurudia mu ma inchi zao. Tunatumikaka juu ya kupata solutions za kudumu ku mashida ya wakimbizi hapa inchini Danemark na fasi zingine duniani.

MSAADA WA KIPESA

- Huu mwaka wa 2019 tuko napatia watu wakubwa 139.274 kr. juu ya kwenda kuanza amo maisha mu inchi yako.
- Tuko napatia watoto 42.476 kr.

Tuko napana izi pesa mu bipindi mbili – pesa za kwanza unazipata wakati ya kuondoka Danemark. Ni 83.565 kr. ku watu wakubwa na 25.486 kr. kwa watoto. Kipindi ya pili ya pesa unaipata ukisha ishi mwaka moja mu inchi yako.

MISAADA ZINGINE ZENYI MUTU ANAWEZA PATA

- Misaada kuhusu safari yenu,
- Misaada ya kuwabebea bitu bienu, wala misaada ya kuuza bingine bitu bienyi munaweza peleka nyumbani,
- Misaada ya kuuza bitu bya kufanya amo kazi nyumbani,
- Kuwalipia assurance ya magonjwa ya miaka 4,
- Kuwauzia madawa za kutumia mwaka muzima,
- Kuwapatia vifaa vya lazima,
- Kulipia watoto wenu masomo miaka 4 batoto benyi biko na umri wa miaka 5 mpaka miaka 16,
- Kuwasaidia kupata vikartasi bya kusafiri.

KAMA ULISHA ENEZA MIAKA 55

Kama ulishaeneza miaka 55, unaweza kuwa napata kila mwezi pesa ya musaada kutoka Danemark.

Musaada ile iko ya 2.800 kr. wala ya 5.500 kr. kila mwezi.

Juu upate hii musaada, inabidi ukuwe ulishaka ishi Danemark miaka 5.

HAKI YA KU RETIRER HII OMBI YA KURUDIA MU INCHI YAKE

Wakimbizi wenyi kutaka, biko na ile haki ya kubadirisha mawazo na kutorudia tena mu inchi yabo. Wana haki pia ya kurudia Danemark mbele mwaka moya iishe kwa wale wenyi walikuwa walisharudia mu inchi yao. Kwa wale wenyi kurudia Danemark, batabarudishia tena haki zabo zote.

Kama mutu anarudia Danemark, itabidi arudishe pesa alipataka za kurudia mu inchi yake.

Wageni wao hawana ile haki ya kurudia Danemark, wakati watakuwa walisha ondoka kutoka Danemark na kupata musaada ya kurudia mu inchi yabo. Ku wageni ni uamuzi wa mwisho, ukisha ondoka kutoka Danemark, nikusema kwaheri kwa zile haki ulikuwaka nazo hapa Danemark, zenyi mutu alikuwaka nazo wakati alikuwa nakaa hapa Danemark.

KAMA UNATAKA KUJUWA MENGI

Kama una nia ya kurudia mu inchi yako, unaweza kututumia fiche ya information yenyi unaweza kupata ku site internet yetu. Wakati tutafanya mukutano na weye, tutakuonesha haki mbali mbali zenyi uko nazo juu uweze kufanya uamuzi. Kama unapenda, tuta alika interprète juu ya ile mukutano. Kazi yetu sisi nikukupatia informations za lazima zenyi zitakusaidia kuamua.

Tutaleta mtafsiri (interprète) ku mukutano, kama unapenda uwe na mtafsiri. Kazi yetu sisi ni kukupatia mashauri ambazo uko nazo lazima juu ufanye uamuzi

Tunapatia watu mashauri Siku ya kwanza mpaka siku ya tano

Kuanzia saa tatu ya asubuyi mpaka saa kenda (9h -15h)

Kidenishi na kingereza

Piga kwa hii simu 33 73 50 00

Kwa izi simu unaweza kupewa mashauri mu luga
– zingine yenyi haiko kidenishi – tena kwa

Kibosnia/ kiserbia / kikroasia

Piga kwa hii simu 33 73 52 33

Kiarabu na kikurdishia (kisorania)

Piga kwa hii simu 33 73 52 28

Kama unapenda mashauri za kipekee kuhusu haki zako
kufwatana na kurudia mu inchi yako, inabidi ujaze
ile fiche ambayo upata ku site internet yetu.

www.flygtning.dk/atvendehjem

www.atvendehjem.dk

Unaweza pia kutuandikia kwa hii email:

atvendehjem@drc.ngo